

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kumb. Na EA.7/96/01/J/169

3 Agosti, 2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi **4 kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.**

1.0 WAKALA WA USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI (RITA)

Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini – RITA ni Wakala wa Serikali ulianzishwa chini ya Sheria ya Bunge Na.30 ya Mwaka 1997 kufuatia Tangazo la Serikali Na. 397 ya tarehe 2/12/2005. RITA ina jukumu la kuhakikisha ufanisi katika usimamizi wa taarifa ya Matukio Muhimu ya Binadamu na Huduma za Ufilisi na Udhamini Tanzania. Wakala unatafuta

1.2 Afisa Usajili Msaidizi Daraja la II– Nafasi (4)

1.3 Majukumu ya kazi ya Afisa Usajili Msaidizi Daraja la II

- i. Kusajili Ndoa, Vizazi na Vifo na Muungano wa Wadhamini na kutunza kumbukumbu zake.
- ii. Kukusanya ada za Ndoa, Vizazi na Vifo na Muungano wa Wadhamini.
- iii. Kutayarisha Fahirisi (Index) za Ndoa, Vizazi na Vifo kwa wilaya na mikoa.
- iv. Kutayarisha matangazo yahasuyo shughuli za mirathi yanayotolewa katika gazeti la Serikali na hati za malipo mbalimbali kuhusu mirathi.
- v. Kutunza magazeti ya Serikali, nyongeza za Sheria (Acts Supplements).
- vi. Kutunza Ratiba za kesi za Mahakamani zinazohusu mirathi (Court Diary) na kuwakumbusha Mwakili wa Serikali wanaohusika.
- vii. Kupokea taarifa na kufanya upekuzi.
- viii. Kuwaelekeza wananchi kuhusu utaratibu wa kuendesha mirathi.

1.4 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye stashada ya Sheria (Diploma in Law)

1.5 MSHAHARA- TGS.C

MASHARITI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka **45**;
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa;
- iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo;**
- iv. **Waombaji** waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika;
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
 - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
 - Computer Certificate
 - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)
 - Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni.
- vi. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA;
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA);
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi;
- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba 2010;
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria;
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 17 Agosti, 2018;
- xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.

Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <http://portal.ajira.go.tz/> (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal')

MUHIMU: KUMBUKA KUAMBATISHA BARUA YAKO YA MAOMBI YA KAZI
ILİYOSAINIWA PAMOJA NA VYETI VYA ELIMU. ANUANI YA BARUA HIYO IELEKEZWE
KWA:

**KATIBU, OFISI YA RAIS,
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**S.L.P 63100
DAR ES SALAAM.**

**LIMETOLEWA NA
KATIBU SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**